


JINZI YA KUSALI ROSARI

1. Ishara ya Msalaba
2. Kanuni ya Imani
3. Atukuzwe Baba
4. Kutangaza Fumbo(Tendo)
5. Baba Yetu
Salamu Maria (10x)
Atukuzwe Baba
6. Salamu Malkia



BABA YETU

Baba yetu uliye Mbiguni, jina lako litukuzwe. Ufalme wako ufike. Utakalo lifanyike duniani kama mbinguni

Utupe leo mkate wetu wa kila siku. Utusamehe makosa yetu, kama tunavyowasamehe na sisi waliyotukosea. Usitutie katika kishawishi, lakini utuopowe maovuni. *Amina.*

SALAMU MARIA

Salamu, Maria, umejaa neema, Bwana yu nawe, umebarikiwa kuliko wanawake wote, na Yesu, mzao wa tumbo lako amebarikiwa.

Maria Mtakatifu, Mama wa Mungu, utuombe sisi wakosefu, sasa na saa wa kufa kwetu. *Amina.*



ATUKUZWE BABA

Atukuzwe Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu. Kama mwanzo, na sasa, na siku zote, na milele. *Amina.*

MAFUMBO YA UTUKUFU

1. Yesu anafufuka.

Yesu, siku ya tatu baada ya kufa kwako, ulifufuka katika wafu. Nao Mitume waliokuona baada ya ufufuko wako walijitolea maisha yao kwa kulinda imani hii. Naamini, pia, kwamba kifo sio mwisho wa maisha.

Nipe neema niwe na roho safi na nyofu, kama yako, ili nifuate njia yako inifikishayo kwa ufufuko na furaha ya milele.

2. Yesu anapaa mbinguni.

Siku arubaini baada ya ufufuko wako, ulipaa mbinguni.

Pia sisi twatamani kuende mbinguni.

Tunataka kuishi kulingana na maadili yako. Lakini hatuwezi hayo bila usaidizi wako.

Tafadhali tupe nguvu ya kustahilisha vipaji Mungu alivyopanda nyoyoni zetu vienee kila siku.

3. Roho Mtakatifu anawashukia Mitume.

Maria, wakati uliomba na Mitume Roho Mtakatifu aliwabadili, wakajawa na ushujaa, na wakaenda kulieneza neno la Yesu lilulikane duniani kote.

Tunaposali rosari, tafadhali omba nasi ili Roho Mtakatifu

afungue milango ya roho zetu. Funza watoto wa dunia ya kisasa kusali rosari na kuishi kwa kukubaliana, ili Roho Mtakatifu awafanye watume wa upendo wa Mungu na wenye furaha.

4. Bikira Maria anapalizwa mbinguni.

Maria, Mungu alikuchukua kwa Moyo na Mwili akakupaliza mbinguni na akakupatia kazi ya kutuleta kwa Yesu, kutuongoza, na kutulinda.

Mama, nakupatia roho yangu.

Nataka kuishi pamoja nawe, na kushirikiana nawe. Nataka roho yako iwe kimbilio na njia yakunipeleka kwa Mungu.

5. Bikira Maria anavikwa Taji kuwa Malkia wa Mbingu na Inchi.

Mama, tunataka kufuata njia yako kama tuifuatayo kwa rosari.

Tunataka kuendelea mbele na maisha tukiwa na nguvu, ustahili, ukarimu, unyenyekevu, na kushirikiana kwa upendo, amani na furaha.

Tunakuvisha Taji uwe Malkia wa roho zetu, na tunakuomba utuongoze na utubadili.

Tunakuomba utusaidie kutafuta Mwanao ili tuwe na furaha.